

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA
MAKUNDI MAALUM**

Simu Na. +255 (026) 2963341/29633446
Nukushi: +255 (026) 2963348
Barua Pepe: ps@jamii.go.tz
Tovuti: www.jamii.go.tz



Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa Afya,
S. L. P 573,
40480 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

**WITO KWA WAFANYABIASHARA NDOGONDOGO KUCHANGAMKIA FURSA YA
MIKOPO YA SERIKALI YENYE RIBA NAFUU.**

Dodoma 30 Januari, 2026

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, inaendelea kutekeleza dhamira yake ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa vitendo.

Kwa muhtadha huo, ninapenda kutumia fursa hii kuwaalika na kuwahamasisha wafanyabiashara ndogondogo wote kuchangamkia **fursa ya mikopo ya Serikali yenye masharti nafuu na riba ya asilimia saba (7%) kwa mwaka** inayotolewa kupitia Benki ya NMB ambayo imeingia makubaliano na Serikali kusimamia mikopo hiyo.

Mikopo hiyo inalenga kuwawezesha **wafanyabiashara ndogondogo wenye mauzo ghafi yasiyozidi Shilingi Milioni Nne (4,000,000) kwa mwaka**, wakiwemo mama na baba lishe, machinga, waendesha bodaboda (magurudumu mawili, matatu na guta), pamoja na makundi mengine yanayotambuliwa na kusajiliwa na Mamlaka husika maeneo mbalimbali nchini.

KUHUSU UTARATIBU; Ili mfanyabiashara ndogondogo aweze kunufaika na mikopo hiyo, anatakiwa awe **ametambuliwa na kusajiliwa kwenye Mfumo wa Utambuzi na Usajili wa Wafanyabiashara Ndogondogo (WBN-MIS)** na Afisa Maendeleo ya Jamii kutoka katika Halmashauri yake; awe ni raia wa Tanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18; awe na biashara inayotambuliwa katika eneo lake au eneo

linalotambuliwa na Mamlaka husika; pamoja na kuwa na Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au Namba ya NIDA.

Aidha, utaratibu wa kuomba mikopo hiyo ni wazi na rafiki ambapo Mwombaji mwenye kitambulisho cha kidijitali au namba ya kitambulisho hicho anatakiwa kufika katika Benki ya NMB kwa ajili ya kujaza fomu ya maombi na kuwasilisha nyaraka zinazohitajika. Maombi yote yanahakikiwa na kuchambuliwa kwa mujibu wa taratibu za benki hiyo na waombaji wanaokidhi vigezo wanaingiziwa fedha kwenye akaunti zao kulingana na aina ya mkopo waliyoomba.

Mikopo hii ina masharti nafuu ikilinganishwa na mikopo ya kibiashara, ambapo **muda wa mkopo ni kuanzia miezi mitatu (3) hadi miezi ishirini na minne (24)** kulingana na aina ya biashara, riba ni **asilimia 7%** tu kwa mwaka, na mkopo umewekewa **bima dhidi ya kifo na ulemavu wa kudumu kwa mkopaji**, kwa lengo la kumlinda mfanyabiashara na familia yake

Nawasihi wafanyabiashara ndogondogo kuchangamkia fursa hii kwa wingi, kwani ni sehemu ya mkakati wa Serikali wa kuongeza mitaji, kukuza biashara zenu, kuongeza ajira, na hatimaye kuboresha maisha ya wananchi na kukuza uchumi jumishi kwa Taifa letu kwa ujumla. Aidha, ninawahimiza wale ambao bado hawajatambuliwa na kusajiliwa kwenye mfumo wa WBN–MIS wafike katika Ofisi za Kata au Halmashauri za Wilaya walipo ili kukamilisha zoezi la utambuzi na usajili.

Serikali itaendelea kushirikiana Benki ya NMB kuhakikisha mikopo hii inawafikia walengwa kwa uwazi, haki na kwa wakati, huku tukisisitiza nidhamu ya marejesho ya fedha ya mikopo ili fursa hiyo iwanufaishe wananchi wengi zaidi.

Mwisho, napenda kuwahakikishia wananchi wote kuwa, Wizara yangu itaendelea kusimamia na kuboresha mifumo ya uwezesaji wananchi kiuchumi, kwa lengo la kujenga Taifa lenye usawa, fursa na ustawi kwa wote.



Dkt. Dorothy Gwajima
**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA
WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**